TANGAZO LA SERIKALI NA. 408 La Tarehe 06/10/2017

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

**SHERIA NDOGO**

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 6(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA ZAO LA KAHAWA) ZA HALMASHAURI YA MJI WA MBINGA ZA MWAKA 2017

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1 Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za ( Ushuru na Usimamizi wa zao la Kahawa) za Halmashauri ya Mji wa Mbinga za mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2 Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Mbinga.

Tafsiri

3 Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo;-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake Afisa yeyote atakayeteuliwa na Halmashauri au Mkurugenzi kwa ajili ya kutekeleza Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Mbinga;

"Jengo" maana yake ni jengo lolote lililojengwa kwa kutumia vifaa vya aina yoyote ile na ni pamoja na jengo lililojengwa kwa kutumia udongo, nyasi na miti, jengo la biashara, makazi, kibanda, kontena, mwavuli uliosimikwa kwa ajili ya shughuli za biashara katika eneo lolote ambalo limeruhusiwa kutumiwa na mtu kibiashara katika eneo la mamlaka ya Halmashauri;

"Kahawa" maana yake ni kahawa kavu iliyokobolewa;

"Kibali" maana yake ni kibali chochote cha maandishi kilichotolewa na Mkurugenzi kwa mtu yeyote anayepata huduma yoyote au mtu anayepata huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"Magoma" maana yake ni biashara haramu ya kununua kahawa ya mkulima kabla ya msimu wa mavuno kwa kumpatia mkopo wa fedha, pembejeo au mali nyingine ili aiuze kwa bei isiyohalali;

"Mazao" au "zao" maana yake ni mazao ya kilimo au misitu, inajumuisha pamoja na nafaka na matunda aina za ndizi mbivu, ndizi za kupika, miwa, matunda aina ya nanasi, machungwa, parachichi, tikiti-maji, maembe na mengineyo yenye asili hiyo;

"Mfanyabiashara" maana yake ni mfanyabiashara yeyote anayeuza bidhaa katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri ikiwa ni pamoja na

mfanyabiashara NdogoNdogo au machinga;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakaye kuwa anatekeleza majukumu ya Mkurugenzi kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"Mtu" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, taasisi au kampuni ambayo inafanya biashara ya aina yoyote katika eneo la Halmashauri;

"Soko" maana yake ni eneo au soko liliotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kama soko kwa ajili ya huduma ya umma;

"Stakabadhi" maana yake ni stakabadhi ya kieletroniki itakayotolewa na Halmashauri kama uthibitisho wa malipo ya ada au ushuru;

"Wakala" maana yake ni taasisi au kampuni iliyoteuliwa au kuingia mkataba na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru au ada kwa niaba ya Halmashauri.

Wajibu wa Halmashauri kusimamia zao la Kahawa

4 (1) Katika kuhamasisha na kusimamia zao la kahawa katika eneo lake Halmashauri itakuwa na wajibu wa:-

(a) Kuhakikisha kuwa wakulima wanasajiliwa pamoja na kiasi cha ekari ya mazao;

(b) Kusimamia upatikanaji wa mbolea na pembejeo za kilimo;

(c) Kuhakikisha upatikanaji wa maafisa ugani

katika kila eneo lake;

(d) Kuhakikisha ubora wa kahawa unazingatiwa na mkulima katika hatua zote za uzalishaji.;

(e) Kuhamasisha uundwaji wa vikundi vya kiuchumi kwa wakulima wa kahawa ili kuhamasisha kilimo cha kisasa;

(f) Kuhakikisha kila mkulima anamuuzia kahawa mnunuzi mwenye kibali cha Halmashauri na leseni ya biashara.

Ushuru wa Kahawa

5 (1) Halmashauri itatoza Ushuru wa zao la kahawa kwa kiwango cha asilimia 3% ya bei ya kununulia zao la kahawa ambao utalipwa na mnunuzi kabla ya kusafirisha zao hilo.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kununua na au kusafirisha zao la kahawa bila kulipia ushuru.

Wajibu wa Wanunuzi wa Kahawa kusajiliwa

6 (1) Wanunuzi wote wanaojishughulisha na ununuzi wa zao la kahawa watapaswa kusajiliwa na Halmashauri ambapo watapatiwa vibali vya kufanya biashara ya zao la kahawa.

(2) Usajili huu utafanyika kila mwaka kabla ya msimu wa zao la kahawa kuanza kwa kulipia kibali cha ununuzi cha Halmashauri.

(3) Kibali kinachotolewa kitamtambulisha mnunuzi, kituo au eneo, kikundi cha wakulima na kiasi ambacho mnunuzi amekubaliwa kununua kwa kipindi kinachoonyeshwa katika kibali hicho.

Wajibu wa wanunuzi

7 (1) Kila mnunuzi atatakiwa kununua zao la kahawa kwa kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hizi.

(2) Kila mnunuzi atanunua zao la kahawa katika kijiji, kata au eneo lolote lililoelekezwa na Halmashauri

ambapo mnunuzi atalipa ushuru unaotakiwa katika eneo alililonunua kahawa.

(3) Kila mnunuzi atasaini Mkataba na Halmashauri utakaomruhusu kununua kahawa na atapewa kibali na Halmashauri.

(4) Itakuwa ni marufuku kwa mnunuzi kununua zao la kahawa bila kuwa na leseni halali ya biashara.

Uuzaji wa kahawa safi

8 (1) Aina ya kahawa inayoruhususiwa ni ya kahawa safi tu.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kujihusisha na biashara ya magoma.

(3) Ununuzi wa zao la kahawa utafanyika kwa mzani au kipimo chochote kingine kilichothibitishwa na Halmashauri.

Usafirishaji wa kahawa

9 (1) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza, kununua na kusafirisha mazao baada ya saa kumi na mbili jioni na kabla ya saa kumi na mbili alfajiri.

(2) Halmashauri itatoa Kibali cha kusafirisha zao la kahawa inayopelekwa nje ya Halmashauri kwa kupewa kibali kama kilivyoanishwa kwenye Jedwali Na.1 la Sheria Ndogo hizi.

Uteuzi wa wakala

10 Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteuwa mtu, Kampuni au Taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria kukusanya Ada au Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa

11 Wakala aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 10 cha

wakala — Sheria Ndogo hizi, atakuwa na wajibu wa:-

(a) Kukusanya na kupokea Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) Wakala atakusanya Ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Makosa kwa wakala

12 Itakuwa ni kosa kwa wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo:-

(1) Atajaribu au atakusanya Ushuru bila idhini ya Halmashauri.

(2) Atajaribu au atakusanya Ushuru kwa kiwango tofauti na kilichoidhinishwa katika Sheria Ndogo hizi.

(3) Atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha Ushuru kilichokubaliwa katika mkataba wa kukusanya Ada au Ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(4) Atashindwa kutoa stakabadhi halali ya kielektroniki ya malipo kwa Ushuru aliokusanya kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Uwezo wa Afisa mwidhiniwa

13 Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote au jengo lolote kwa nia ya kukusanya, kufanya tathimini au jambo lolote linalohusiana na Ushuru, Leseni au Kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa

14 Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo mtu yeyote:-
Atashindwa , atadharau , atakwepa au atakataa

(1) kulipa Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ushuru.

(3) Atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(4) Atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ushuru ndani ya Halmashauri.

(5) Atashindwa au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa Ushuru.

(6) Atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya Ada au Ushuru.

(7) Atajihusisha na biashara ya magoma.

Adhabu

15 Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/= na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miaka miwili (2) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

16 Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa.

---

JEDWALI LA KWANZA

---

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 9 (2))*

HATI YA USAFIRISHAJI KAHAWA KWENDA NJE YA HALMASHAURI YA MJI WA MBINGA

1. Jina la Mnunuzi/Kampuni/AMCOS….……………………………………..
2. Aina ya kahawa inayosafirishwa……….kg………idadi ya magunia……..
3. Zao linasafirishwa kutoka kiwanda/ghala……………….………………….
4. Kwenda Mkoa/Wilaya……………………………………………………
5. Jina na anuani ya mwenye gari…………………….……………………..

   Namba ya gari………………………………….………………………
6. (a) jina la Dereva/msafirishaji…………………….…...……………..

   (b)saini ya dereva/msafirishaji…………………………………….……..

   (c) namba ya leseni ya dereva......................................................….........
7. Afisa mkaguzi<br>Jina……………….…………saini…………………..tarehe…………….
8. Hati imetolewa na:<br>Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga

   Jina…………………………..……..saini………………….…………

   Tarehe..................................................muhuri………………..………..

   Nakala kwa:-

   Kizuizi/geti la ukaguzi

   Hati itatumika kwa muda wa siku moja tu.

JEDWALI LA PILI

KUFIFILISHA KOSA

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 16)*

Mimi……………………………………..nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya………………………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga kwamba mnamo tarehe……ya mwezi……………..mwaka ………….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ………………………cha Sheria Ndogo za (Ushuru na Usimamizi wa zao la Kahawa) za Halmashauri ya Mji wa Mbinga za mwaka 2016.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninachodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………………ya mwezi…………………Mwaka………………………..

Jina…………………………………..

Saini………………………………….

Mbele ya:

Jina………………………………………..

Cheo………………………………………

Saini……………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Mji Mbinga imebandikwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 9 ya mwezi Februari mwaka 2017 mbele ya:-

ROBERT KADASO MAGENI,
*Mkurugenzi wa Mji*
*Halmashauri ya Mbinga*

NDUNGURU EGNO KIPWELE,
*Mwenyekiti wa Halmashauri*
*Mji wa mbinga*

NAKUBALI,

Dodoma,
August, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB.),
*Waziri wa Nchi - OR - Tamisemi*